


kuangika chombo cha "Tippy Tap" kwenye choo au nje.
Chombo hicho cha "Tippy Tap" kiko tayari kutumika.

JINSI YA KUTUMIA "TIPPY TAP"


- Pitisha maji kwa mikono.
- Tumia sabuni.
- Tumia maji safi kutoa pofu ya sabuni.
- Tumia kitambaa kwa kufutia mikono.



REAP,
P.O. Box 21083,
Ngong Road,
Nairobi, 00505,
Kenya.

CHOMBO CHA "TIPPY TAP"

Ukosefu wa maji ndicho kiini muhimu ambacho huwafanya watu kukosa kuosha mikono yao kila mara.




Hapa kuna njia ambayo hutumia sehemu moja kwa kumi ya maji tunayotumia kuosha mikono. Chombo cha "Tippy Tap"


hutengenezwa kwa kibuyu cha plastic kilicho na shimo katika mkono wake. Kwa kunawa mikono unahitaji sabuni, kwa hivyo inafungwa kwa kamba na hukingwa isinyeshewe na kuwa majimaji.

JINSI YA KUTENGENEZA CHOMBO CHA "TIPPY TAP"

1. Kwa uangalifu chemsha chini ya mkono wa kibuyu juu ya mshuma au taa ya koroboi. Zungusha mkono hadi uanze kushika moto na kuwa mwepesi kotekote.




2. Toa mshuma au koroboi na haraka finya hapo chini ya mkono wa kibuyu kwa kutumia "pliers" ili ishikane kabisa na kuzuia maji yasipite. Shikilia "pliers" hapo mpaka patakapo poa, ukiangalia yakwamba hapo mahali pameshikana kabisa.



3. Chemsha sehemu kidogo ya msumari juu ya mshumaa. Tumia msumari moto kwa kutoboa shimo nje ya mkono wa kibuyu, hatua chache juu ya ile sehemu iliyo shikanisha.

4. Chemsha msumari tena na tumia kwa kutoboa mashimo mawili kubwa kidogo nyuma ya kibuyu na yawe katikati, na pia kuachana upana wa kidole cha gumba na kile cha pete.



5. Funga kamba ili ipitie kwa hizo shimo mbili na ufunge mwisho wake kwa miti au kijiti. Toboa sabuni ya kipande na kifuniko na ufunge kwa kamba ingine. Kifuniko cha mkebe hukinga sabuni kwa mvua na jua. Unganisha hii kwa mojawapo ya zile kamba zilizofungwa kwa miti au kijiti.

6. Funga kamba nyingine ikizunguka mdomo wa kibuyu na uiaache ikining'inia. Kamba hii hutumia kuvuta chombo cha "Tippy Tap" ili maji yaweze kudondoka kutoka kwa lile shimo, iliyotengenezwa katika mkono wa kibuyu.

7. Jaza maji kwenye chombo cha "Tippy Tap" mpaka kufikia kile kiwango cha kamba iliyotengenezwa nyuma ya kibuyu. Tumia mti au kijiti ambacho umetengeneza kwa